**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**
**MTIHANI WA UTALIMILIFU DARASA LA IV**
**SOMO: KISWAHILI**

**Muda: saa 1:00 Jina la Mtahiniwa:………………………………….…………..**

## SEHEMU A: (Alama 20)

LUSAELIMU.COM

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

**1.Sikiliza kwa makini sentensi zitakazosomwa na Msimamizi kisha ziandike kwa usahihi.**

i. ……………………………………………………………………………………
ii. ……………………………………………………………………………………
iii. ……………………………………………………………………………………
iv. ……………………………………………………………………………………
v. ……………………………………………………………………………………

**2. Katika kipengele cha (i) – (x), chagua jibu sahihi na uandike herufi ya jibu hilo katika mabano uliyopewa.**

i. Mafundi wa mradi wa maji walichimba kisima …………….. siku mbili. A. ya B. kwa C. na D. la ( )

ii. Sisi tunacheza mpira wa miguu. Sentensi hii ipo katika wakati gani? A. wakati uliopita B. wakati ujao. C. wakati uliopo. D. wakati uliopo timilifu. ( )


iii. Babu yetu hutusimulia hadithi na kufanya maigizo mbalimbali ambayo hutufanya tujifunze vitu vingi pamoja na kuburudika. Je, mtu anaye simulia hadithi au kuigiza maigizo kisanaa huitwa: A. hadhira B. msemaji C. mfundishaji D. fanani ( )

iv. Seremala …………………………. kinyago kizuri. A. alichongesha B. alichonga C. alifinyanga D. alikichongesha ( )

v. Wanafunzi wa darasa la nne ………………… mbuga ya Serengeti. A. walidhuru B. walizuru C. waliduru D. walizulu ( )

vi. Kipi ni kipande cha pili kinacho kamilisha methali hii, "Ngoja ngoja ……………………………….." A. hujaza tumbo B. huvimbisha tumbo C. huumiza tumbo D. huleta uvumilivu ( )

vii. Kipande cha kwanza cha methali hii ni kipi, "………….. si chururu". A. kidogokidogo B. ndondondo C. haba na haba D. nenenene ( )

viii. 
Kitendawili kipi kinajibiwa na picha hiyo? A. ana mdomo wa chuma B. ana mdomo lakini anauma kwa mkia C. ana miguu ya msumeno D. vita vya panzi furaha ya kunguru ( )

ix. Gari lilikata kulia kuelekea ukumbini. Kinyume cha neno kulia ni kipi? A. kushoto B. nyuma C. mbele D. kutoa machozi ( )

x. Asha ni mtoto wa kwanza kuzaliwa kwa wazazi wake. Je, Asha tunamwitaje kwa kuwa mtoto wa kwanza kuzaliwa? A. kitindamimba B. kifungamimba C. kilindamimba D. kifunguamimba ( )

## SEHEMU B: (Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. **Panga herufi zilizochanganywa katika kipengele cha (i) – (v) ili kuunda maneno sahihi ya Kiswahili.**
i. DIHATHI ………………………….……………..
ii. PAHO ………………………………………..
iii. MINAZA ……………………………………….
iv. JAPAMO ………………………………………
v. KAWAPU ………………………………………...

4. **Zipange sentensi zifuatazo ili kupata kifungu cha habari chenye maana kwa kuzipa herufi A-E.**
i. Hutandika vitanda vyao, huoga na kuvaa sare za shule. (  )
ii. Hunywa chai na kwenda shuleni. (  )
iii. Huamka mapema kila siku asubuhi. (  )
iv. Baada ya masomo hurudi nyumbani. (  )
v. Jamali, Hamisi na Rehema wanasoma Darasa la nne. (  )

**SEHEMU C Alama 10**

Jibu swali la **tano** (5)

5. **Soma kwa makini habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.**

Paulina ni mwanafunzi wa shule ya msingi Mpitimbi. Anapenda kusoma na marafiki zake Mboni, Baraka na Tumaini. Wakati wa kufunga shule alitangazwa kuwa mshindi wa kwanza katika darasa lao. Alishtuka na kusema, Aha! Nmewashinda wote. Ndoto ya Paulina ni kusoma hadi chuo kikuu na kuwa rubani. Paulina ni mwanafunzi anayejitambua na mwenye kuweka malengo ya baadaye. Wewe je?

**MASWALI**

i. Shule anayosoma Paulina inaitwaje? …………………………………….
ii. Wapi ni marafiki zake Paulina? …………………………………………
iii. Alishtuka na kusema, Aha! Neno "Aha!" ni alama gani ya uandishi imetumika? …………………………………………………………………...
iv. Paulina ana ndoto ya kuwa rubani. Je, rubani ni mtu anayefanya kazi gani? ……………………………………………………………………..
v. Kinyume cha "marafiki" ni kipi? ……………………………………..

**IFAKARA TOWN COUNCIL**
**MOCK EXAMINATION STD IV**
**SUBJECT: ENGLISH LANGUAGE**

**Time: 1:00 Hour Candidate's name:**…………………………………………………..

## SECTION A 30 MARKS

LUSAELIMU.COM

Answer **all** questions in this section.

**1. Listen carefully the sentences read by your invigilator then write them correctly in the space provided**

i. ……………………………………………………………………………

ii. ……………………………………………………………………………

iii. ……………………………………………………………………………

iv. ……………………………………………………………………………

v. ……………………………………………………………………………

**2. Choose the most correct answer from the given alternatives and write its letter in the box provided.**

i. My brother flies an aeroplane. Therefore, he is a …………. A. doctor B. tailor C. pilot D. fishman ( )

ii. ……………… is the meal we take in the afternoon A. breakfast B. lunch C. dinner D. brunch ( )

iii. If the plural form of you is you, what is the plural form of "she"? A. shes B. shees C. they D. hers ( )

iv. The son of your aunt is your ……………………. A. uncle B. cousin C. nephew D. father ( )

v. We …………. on the bed. A. cook B. dig C. sit D. sleep ( )

vi. Our English teacher ……………. us to study hard every day. A. tell B. tells C. telling D. told ( )

vii. Last week, our team, Dreams FC ………………………….... the match. A. win B. won C. wins D. wined ( )

viii. When I arrived there, she warmly ………………… me at her house. A. welcome B. welcome C. welcomed D. welcome ( )

ix. It was …………………………………. when I slept. A. rain B. shall rains C. raining D. been raining ( )

x. He failed the English examination, ………………………….. he did not study hard. A.so B. because C. but D. and ( )

**3. Match the words from the list A and the words with similar sounds in list B by writing the letter of the correct answer.**

| No. | LIST A | ANSWER | LIST B |
|---|---|---|---|
| i. | Sea | ( ) | A. Meet |
| ii. | Right | ( ) | B. Buy |
| iii. | Meat | ( ) | C. Knew |
| iv. | New | ( ) | D. See |
| v. | Bye | ( ) | E. Write |

## SECTION B: (10 MARKS)

**Answer all questions in this section**

4. **Write the correct English word from the jumbled letters in the brackets to make meaningful sentences.**

i. She is a (odog) ……………..………………… girl in our school.

ii. Mary (newt) ………………..………. to Dar es salaam last week.

iii. She (rtowe) ………………………...………………….. an email.

5. **Complete the following John's daily routine by writing the verbs in the brackets into correct form.**

John (i) …………………… (wake up) early in the morning every day. He (ii) ……………………………. (brush) his teeth. Then he (iii) …………………… (go) in the garden for watering flower, vegetables and fruit trees. After finishing, he (iv) ……………………….. (come) back to home for breakfast.

**SECTION C: (10 marks)**
**Answer question six (6)**

6. **Read the following passage carefully and then answer the questions that follow.**

My name is Angel. I am in class four. I go to school at Twendepamoja primary school. My family has five members, my father, my mother, my brother, my young sister and I. My father's name is Masanja. My mother's name is Sikujua. My brother's name is Jacob. My young sister's name is Agnes.

**QUESTIONS**

i. What is the name of Angel's school? …………………………….

ii. Angel's family has …………………………………….  members.

iii. What is the name of Angel's mother? …………………………..

iv. The young sister of Angel is called ………………………………

v. Masanja is Angel's ……………………………………………….

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**
**MTIHANI WA UTALIMILIFU DARASA LA IV**
**SOMO: HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**
**Muda: saa 1:00 Jina la Mtahiniwa:……………………………………..…..**

**SEHEMU A: (Alama 20)**
Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. **Katika kipengele cha i - x, chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku ulichopewa.**

i. Maadili yaliisadia jamii kuishi katika misingi ipi? A. uonevu na ubaguzi B. dhuluma na unyonyaji C. upendo na heshima D. chuki na umoja ( )
ii. Lipi ni tendo lisilo la kuwajali wengine kati ya haya yafuatayo? A. kuwasaidia wazee B. kuwatazama wagonjwa C. kuwatunza wasiojiweza D. kutokutembea usiku ( )
iii. Maadili yalisimamiwa vizuri katika kila nyanja ya kimaisha katika jamii za kale. Je, jambo lipi ni miongoni wa maadili yaliyokuwepo katika dini? A. kusimama B. kupiga magoti C. kucheza D. kusoma ( )
iv. Rushwa ni kitendo kinachopigwa sana vita katika jamii kutokana na athari zake. Je, ipi ni athari mojawapo ya kitendo hicho katika jamii. A. matumizi bora ya rasilimali B. kuboresha miundombinu ya jamii C. migogoro na ukiukwaji wa haki za binadamu D. kujenga shule nzuri. ( )
v. Jamii za kale ziliamini uwepo wa miungu iliyokuwa na nguvu za kutatua matatizo yasiyowezekana katika jamii kwa kufanya ibada mbalimbali. Je, ipi siyo sehemu mojawapo ambayo ibada hizo zilifanyika? A. nyumbani B. makaburini C. chini ya miti mikubwa D. mapangoni ( )
vi. Mienendo, taratibu au kanuni za jamii zinazotendwa mara kwa mara huitwaje? A. maadili B. mila C. utamaduni D. desturi ( )
vii. Elimu kabla ya ukoloni ilitolewa kwa kuzingatia nini? A. shughuli za jamii na mazingira B. wingi wa watu katika jamii husika C. uvuvi D. uwindaji ( )
viii. Jamii nyingi za kale kabla ya ukoloni zilikuwa na utawala wa kimamlaka ambazo zilijulikana kama tawala za kijadi. Je, jamii ya wahehe iliongozwa na kiongozi yupi wa kijadii? A. mtemi Isike B. Mtemi Mirambo C. Mangi Sina D. Mutwa Mkwawa ( )
ix. Shughuli ya kuvuna samaki kutoka mtoni, bwawani au baharini inaitwaje? A. kilimo B. uwindaji C. uvuvi D. ufinyanzi ( )
x. Jamii za kale zilitumia maarifa na ujuzi tofautitofauti katika kuwinda. Je, ni mnyama yupi alitumika katika uwindaji? A. paka B. mbwa C. mbuzi D. ng'ombe ( )

2. **Oanisha maneno ya fungu A na yale ya fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi zaidi ili kupata maana iliyo kamili.**

| FUNGU A | JIBU | FUNGU B |
|---|---|---|
| i. Msimamizi mkuu wa majukumu ya viranja | ( ) | A. Kiranja wa taaluma |
| ii. Katibu wa vikao vya kamati ya Taaluma | ( ) | B. Kiranja mkuu |
| iii. Katibu wa vikao vya kamati ya shule | ( ) | C. Kamati ya shule |
| iv. Mwanafunzi anayefuatilia ufundishaji na ujifunzaji darasani | ( ) | D. Mwalimu mkuu msaidizi<br>E. Mwalimu wa taaluma |
| v. Ngazi ya juu kabisa ya uongozi wa shule. | ( ) | F. Mwalimu Mkuu<br>G. Kiranja wa nidhamu |


3. **Jibu vipengele i - v kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.**

i. Mavazi ya heshima katika jamii ni ya namna gani? ……………………………… (yanayositiri mwili, yanayoonesha maungo ya mwili, yanayofunika macho)
ii. Mabaki ya majengo ya kale yanayoonekana mpaka leo yanaitwaje? ……………………………………………………… (majumba, masalia, magofu)
iii. Hali ya kupenda nchi au jamii kwa kuweka maslahi yake kwanza zaidi ya maslahi yako binafsi huitwaje? ……………………… (uzalendo, utu, mhanga)
iv. Kutii sheria za nchi, kulinda mali za umma ni mojawapo ya kutimiza ……………………………………..….. katika jamii. (haki, upendo, wajibu)
v. Msaidizi wa Mwalimu Mkuu katika maswala ya utawala ni ………………… (Mwalimu Mkuu msaidizi, Mwalimu wa Taaluma, Daka mkuu)

**SEHEMU B: ALAMA 18**
Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

**4. Chunguza kielelezo kifuatacho cha mti wa familia kisha jibu maswali yanayofuata katika kipengele cha i-v.**

LUSAELIMU.COM




i. Familia inayoonekana katika mchoro huo inaundwa na jumla ya watu wangapi? ………….
ii. Katika familia hiyo kuna watoto wangapi? ……………………………………………….………
iii. Daudi anawaita jina gani **Anna** na **Jenipha** linalowakilisha uhusiano wao kama wanafamilia? ……………………………………………………………………………………………..
iv. Anna, Daudi na Jenipha wanawaita jina gani **baba** na **mama** linalowakilisha uhusiano wao kama wanafamilia? ……………………………………………………………………………………..

**5. Chunguza picha ifuatayo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.**



**Maswali**

i. Picha hiyo inaonesha mazingira gani? …………...
ii. Katika picha hiyo watoto wanapata haki gani? ……………………………………………………….
iii. Je, watoto wanawajibu upi katika mazingira hayo kwenye picha? ……………………………
iv. Ni kitendo gani kinafanyika katika picha hiyo? ………………………………………………
v. Ipi ni faida ya kitendo kinachofanyika katika picha hiyo? ………………………………………..

**SEHEMU C: ALAMA 12**

Jibu swali la sita 6

**6. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu swali.**

Ukoo ni kundi la watu wanaohusiana kwa damu, ambao kwa kawaida wanatokana na babu au bibi mmoja wa ukoo huo. Ukoo hujumuisha vizazi mbalimbali vinavyotokana na asili moja. Katika jamii nyingi, ukoo ni msingi muhimu wa utambulisho, urithi, na mshikamano wa kifamilia. Ukoo unaweza kuwa wa upande wa baba (ukoo wa baba) au upande wa mama (ukoo wa mama). Jamii nyingi barani Afrika hutumia mfumo wa ukoo wa baba ambapo watoto hutambulika kwa jina au ukoo wa baba yao. Hata hivyo, kuna jamii pia zinazo tambua ukoo wa mama. Majukumu ya ukoo ni pamoja na kusaidiana wakati wa shida, kushirikiana kwenye shughuli za kifamilia kama harusi, misiba na mila mbalimbali, pamoja na kutoa mwelekeo wa maadili kwa wanachama wake. Pia ukoo huhusika katika kutoa urithi na kupanga ndoa au kutoa ushauri wa kifamilia. Ni muhimu kwa kila mtu kuutambua ukoo wake, kwani husaidia kujua historia ya familia na kuepuka kuoana na mtu wa ukoo mmoja, jambo ambalo halikubaliki katika tamaduni nyingi.

**Maswali**

i. Kundi la watu wanaohusiana kwa damu, ambao kwa kawaida wanatokana na babu au bibi mmoja huitwa. ……………………………………………………………….……………………………..
ii. Ukoo hujumuisha vizazi mbalimbali vinavyotokana na nini? ……………………………………..
iii. Taja majukumu mawili tu ya ukoo; ………………………………. na ……….……………………..
iv. Taja shughuli mbili tu za kifamilia ambazo koo huweza kushirikiana. …………………………
v. Kwanini ni muhimu kila mtu kuutambua ukoo wake? …………..…………………….……………...…
vi. Jamii nyingi barani Afrika hutumia mfumo upi wa ukoo? ……………………………………….

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**
**MTIHANI WA UTALIMILIFU DARASA LA IV**
**SOMO: JIOGRAFIA NA MAZINGIRA NA SANAA NA MICHEZO**

**Muda: saa 1:00      Jina la Mtahiniwa:..........................................................................................**

**SEHEMU A: JIOGRAFIA NA MAZINGIRA (ALAMA 26)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. **Katika kipengele cha (i) - (vi), chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku ulichopewa.**

i. Samaki huweza kuvunwa kwa njia mbalimbali kutoka majini. Je, ni kwa nini uvuvi wa kutumia nyavu za kokoro ni haramu? A. huvua samaki wengi B. huharibu mazalia ya samaki C. huharibu vyanzo vya maji D. huvua samaki wachache (   )

ii. Ikiwa mjomba wako amenunua eneo kubwa lenye msitu, utamshauri afanye shughuli gani za uzalishaji? A. uvuvi na ufugaji B. upasuaji wa mbao na ufugaji wa nyuki C. kilimo cha umwagiliaji na utalii D. uchimbani wa madini na utalii (   )

iii. Ipi ni mojawapo ya njia zinazoweza kutumika ili kuwa na kilimo endelevu bila kuharibu ardhi? A. kutumia samadi B. kulima kilimo cha kuhamahama C. kutumia madawa ya kikemikali ya kuulia wadudu na magugu D. kutumia mbolea za viwandani (   )

iv. Iwapo unaona doti nyingi zilizokaribiana kwenye ramani, inamaanisha nini? A. kuna watu wachache B. kuna watu wengi C. kuna miti mingi D. kuna maji mengi (   )

v. Ipi ni njia mojawapo mbadala inayoweza kusaidia kupunguza uchafuzi wa hewa? A. kutumia gesi na umeme B. kutumia kuni C. kutumia mkaa D. kutumia magari yanayotumia mafuta kama vile petrol na dizeli (fueli) (   )

vi. Miti ni mojawapo ya vitu vinavyosafisha mazingira ya hewa. Je, ni kwa namna gani miti inasafisha hewa? A. miti hupunguza oksijeni hewani B. miti huongeza moshi hewani C. miti hupunguza maji hewani D. miti hupunguza hewaukaa (   )

2. **Chagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

| | | |
|---|---|---|
| Kaskazini | Kusini | Mawio Na Machweo Ya Jua |
| Mashariki | Magharibi | Asubuhi |

i. Njia ya kubaini pande kuu za dunia kwa kuangalia jua linapochomoza au linapozama hujulikana kwa jina gani? ……………………………………………………………………

ii. Wakati wa asubuhi, ukisimama kwa kulitazama jua upande huo ni upi wa dunia? …………………………………………………………………………………………………..

iii. Wakati wa jioni ukilitazama jua linapozama, kulia kwako kutakuwa upande gani wa dunia? ……………………………………………………………………………………

iv. Jonathan aliondoka nyumbani kwao asubuhi kuelekea shuleni ambako uelekeo wake ndio jua linakochomoza na kivuli chake kilikuwa nyuma yake. Je, uelekeo wa kivuli cha Jonathan ulikuwa ni upande gani wa dunia? ……………………………………………

3. **Jaza nafasi zilizo achwa wazi katika kipengele cha (i) – (iv).**

i. Uchoraji wa ramani ni sanaa na sayansi ya kuonesha kwenye karatasi au uso bapa mahali ambapo vitu vinapatikana katika uso wa dunia. Je, taaluma ya uchoraji wa ramani huitwaje? ……………………………………………………………………………

ii. Mtu anaye jishughulisha na uchoraji wa ramani huitwaje? ……………………………

iii. Michoro midogo inayotumika kwenye ramani kuwakilisha vitu halisi huitwa. …………………………………………………………………………………………………..

iv. Taja program mbili tu zinazoweza kutumika kuchorea ramani kidigitali. ……………………………………………… na ……………………………………………...

4. **Chunguza ramani ifuatayo ya Kijiji cha Mto wa mbu kisha jibu maswali yanayofuata.**




**Maswali**

i. Je, katika kata ya Sinza kuna misikiti mingapi? ……………………
ii. Katika ramani hiyo kuna makanisa mangapi? ……………………………..
iii. Katika ramani hiyo Kijitonyama ipo upande gani mwa Manzese? ………
iv. Katika kata ya Sinza hiyo katika ramani kuna ofisi za umma ngapi? …………………………………………

**SEHEMU B: SANAA NA MICHEZO (ALAMA 24)**
**Jibu maswali yote katika sehemu hii.**

i. **Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi na andika herufi yake katika mabano.** Maumbo ya ukumbi kama vile maumbo ya mchemraba, mchemstatili, mcheduara na piradidi hufinyangwa kwa njia ipi? A. njia ya pindi B. njia ya bapa C. njia ya kufinyafinya D. njia ya kufinya ( )
ii. Sanaa ambayo hutumia michoro kama lugha iliyokamilika ambayo wanaweza kuiona na kuielewa hata kama hawajui kusoma na kuandika huitwa. A. uimbaji B. ususi C. uchongaji D. uchoraji ( )
iii. Je, mavazi ya waigizaji kwenye sanaa za maonesho huitwaje? A. Maleba B. Mapambo C. Makunzi D. maigizio ( )
iv. Je, ni kundi gani linawakilisha ala za muziki za kupuliza? A. Ngoma, marimba na filimbi B. Kayamba, manyanga na ngoma C. Tarumbeta, filimbi na baragumu D. manyanga, ngoma na baragumu ( )

5. **Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuchagua jibu sahihi katika kisanduku na kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

| | | |
|---|---|---|
| Toni | kuinua na kushusha mabega | kuangalia chini |
| koni | noti | puto | kigimbi |

i. Mwondoko wa mwili ambao hufanywa na mwigizaji kuonesha hisia za kutojiamini, kuogopa au aibu. ………………………………………………………………………………..
ii. Alama za maandishi zinazotumika katika muziki kuwakilisha sauti fulani. ………….
iii. Mwondoko ambao ukifanywa na mwigizaji huonesha hisia za kutojali, kukubali kushindwa au kutokuwa na uhakika. ………………………………………………………
iv. Kifaa cha plastiki chenye umbo la pia kinachotumika kuweka mipaka kwenye mazoezi ya wachezaji wa mpira huitwa. …………………………………………………
v. ……………………………………………… ni sauti yenye kipimo maalumu na ubora.

6. **Mazoezi ya viungo hufanyika kwa malengo mbalimbali ikiwemo mtindo wa maisha wenye kujenga afya.**
i. Taja zoezi moja unaloweza kulifanya kwa ajili ya kujenga unyumbufu wa mwili. ………….
ii. Taja zoezi moja unaloweza kulifanya kwa ajili ya kujenga uratibu wa mwili. ………………..

7. **Chunguza picha ifuatayo kisha jibu maswali katika kipengele cha (i) na (ii) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.**



**Maswali**
i. Mchezo huo unaitwaje ……………………………………
ii. Katika mchezo huo kuna namna mbili ambazo kijiko huweza kuwekwa. Zitaje namna hizo. (a)……………………………(b)……………………………..
iii. Mchezo huo huweza kusaidia kuimarisha kitu gani katika mwili? ……………………………………..……..

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**
**MTIHANI WA UTALIMILIFU DARASA LA IV**
**SOMO: HISABATI**

**Muda: saa 1:00 Jina la Mtahiniwa:………………………………………………….**

**SEHEMU A: (Alama 36)**




| | SWALI | KAZI NA JIBU |
|---|---|---|
| 1. i. | Andika 28304 kwa tarakimu. | |
| ii. | Andika tarakimu inayowakilisha makumi elfu katika namba 580247. | |
| iii. | Katika namba 61374 ni tarakimu ipi ina thamani sawa na 50 + 20? | |
| iv. | Andika kwa kirefu 405. | |
| v. | Andika XCI kwa namba za kiarbu. | |
| vi. | Ni namba ipi inafuata katika mfululizo wa namba X, XIV, XVIII, ………………… | |
| 2. i. | 8 6 6 1 3 6<br>+ 7 2 9 2 8 | |
| ii. | 5 8 8 3 4<br>- 9 2 5 4 | |
| iii. | 2 1 3<br>x 5 | |
| iv. | $812 \div 4 =$ | |
| v. | 764 + 92 = | |

| | | |
|---|---|---|
| 3 i. | $\frac{1}{8} + \frac{4}{8} =$ | |
| ii. | $\frac{3}{5} + \frac{1}{5} - \frac{2}{5} =$ | |
| iii. | Kuna $\frac{1}{4}$ ngapi katika kitu kizima kimoja? | |

| | | |
|---|---|---|
| 4 i. | Badili kilogramu 6 kuwa gramu. | |
| ii. | Watoto watatu walikunywa lita 1 ya maziwa siku ya jana na leo wamekunywa lita 2 za maziwa. Je, watoto hao wamekunywa | |

| | | |
|---|---|---|
| | mililita ngapi za maziwa kwa jana na leo? | |
| iii. | Umbali kati ya vijiji viwili ni meta 8000. Je, umbali huo ni sawa na kilometa ngapi? | |
| iv. | Andika saa mbili na nusu kwa tarakimu. | |

**SEHEMU B: (Alama 14)**

| | | |
|---|---|---|
| 5 i. | Watoto 4 waligawana pipi walizopewa na shangazi yao kwa idadi sawa. Ikiwa kila mtoto alipata pipi 8 je, pipi walizogawana zilikuwa ngapi? | |
| ii. | Ukizidisha namba fulani kwa 4 jibu linakuwa 20. Je, hiyo namba fulani ni ipi? | |
| iii. | Paulo alipanda miche 36 siku ya kwanza na akapanda miche mingine siku ya pili. Kama jumla ya miche aliyopanda kwa siku zote mbili ni 70 je, siku ya pili alipanda miche mingapi? | |
| 6 i. | Tafuta mzingo wa pembetatu ifuatayo.   | |
| ii. | Bustani ya shule ina umbo la mraba. Ikiwa mzingo wa bustani hiyo ni mita 40, tafuta urefu wa upande mmoja wa bustani hiyo. | |
| iii. | Taja jina la umbo lifuatalo.  | |
| iv. | Tafuta eneo la mstatili ufuatao.   | |

LUSAELIMU.COM

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA**
**MTIHANI WA UTALIMILIFU DARASA LA IV**
**SOMO: SAYANSI**

**Muda: saa 1:00 Jina la Mtahiniwa:……………………………………………….**

**SEHEMU A: ALAMA 22**

**1. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.**

i. Binadamu ana milango mingapi ya fahamu?
A. saba B. miwili C. mitano D. mitatu ( )

ii. Utabiri wa awali wa matokeo ya uchunguzi wa kisayansi huitwaje?
A. jaribio B. hitimisho C. kubaini tatizo D. dhanio ( )

iii. Kazi ya kufyonza maji na virutubisho kutoka kwenye udongo katika mmea hufanywa na sehemu gani ya mmea?
A. mizizi B. majani C. shina D. maua ( )

iv. Nini kazi ya oksijeni katika mchakato wa uunguaji wa vitu? A. kutoa joto B. kuzuia moto C. kuchochea moto kuwaka D. kugeuza kuni kuwa majivu ( )

v. Joto husafiri kwa njia gani katika kipande cha chuma?
A. mnururisho B. msafara C. mvukizo D. mpitisho ( )

**2. Oanisha ugonjwa kutoka fungu A na maelezo yake fungu B ili kupata sentensi sahihi.**

| FUNGU A | JIBU | FUNGU B |
|---|---|---|
| i. Saratani | ( ) | A. Ugonjwa unaosababishwa na vimelea vya plasimodiam |
| ii. Malaria | ( ) | B. Ugonjwa wa kuharisha na kutapika unaosababishwa na kula chakula au kunywa maji yenye vimelea vya ugonjwa huo. |
| iii. Kipindupindu | ( ) | C. Ugonjwa wa kuambukiza unaoathiri zaidi mapafu |
| iv. Kisukari | ( ) | D. Ugonjwa usio wa kuambukiza unaotokea kwenye chembe hai za mwili wa binadamu. |
| v. Kifua kikuu | ( ) | E. Ugonjwa unaosababishwa na mwili kushindwa kudhibiti kiwango cha sukari |

**3. Chagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kujaza nafasi iliyo wazi.**

| | | |
|---|---|---|
| Kabohaidreti au wanga | Protini | Vitamini na madini |
| Mafuta | Magimbi na viazi mbatata | nyama na samaki |

i. Kundi la vyakula vya kujenga mwili ……………………………………….
ii. Kundi la vyakula vya kulinda mwili. ……………………………………..
iii. Kundi la vyakula vya kuupatia mwili nguvu ……………………………
iv. Kundi la vyakula vya kuupatia mwili joto ……………………………
v. Vyakula katika kundi la protini ……………………………………………
vi. Vyakula katika kundi la wanga ……………………………………………

## SEHEMU B: ALAMA 28

**4. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.**

Mamalia ni moja ya kundi la wanyama kati ya makundi matano ya wanyama wenye uti wa mgongo (vertebrates). Sifa kuu zinazowatofautisha mamalia na wanyama wengine ni kama ifuatavyo. Kunyonya maziwa watoto wao. Watoto wa mamalia hunyonya maziwa kutoka kwa mama yao. Nywele au manyoya. Mamalia wote wana nywele au manyoya katika hatua fulani ya maisha yao, hata kama ni kidogo. Joto la mwili thabiti. Mamalia huweza kudhibiti joto la mwili wao, bila kutegemea mazingira ya nje. Kwa mfano joto la kawaida la mwili wa binadamu ni nyuzijoto za sentigredi 37. Kuzaa watoto walio hai. Mamalia huzaa watoto walio hai tofauti na wanyama kama ndege au samaki wanaotaga mayai. Mamalia hupumya kwa kutumia mapafu na wana moyo uliogawanyika katika vyumba vine. Mamalia wamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni mamalia wa ardhini, mfano tembo, mbwa, paka na binadamu, mamalia wa majini, mfano pomboo na nyangumi na mamalia wanaoruka, mfano ni popo.

**Maswali**

i. Kuna makundi mangapi ya wanyama wenye uti wa mgongo? ………………………………………………………………………………………...

ii. Mfano wa mamalia wanaoruka ni mnyama gani? …………………………………

iii. Mamalia hupataje watoto? ……………………………………………………………….

iv. Mamalia hupumua kwa kutumia nini? ……………………………………………….

v. Joto la mwili wa binadamu ni nyuzi joto za sentigredi ngapi? ……………………

**5. Toa maana ya kila alama ya usalama katika alama hizo hapo chini.**





**……………………**　　**…………………………**



**………………………….**







**…………………………..**　**……..………………………..**　**………………………..**

**6. Jibu maswali yafuatayo.**

i. Bainisha faida moja ya kutumia michezo sahili katika kujifunza. …………………………………………………………………………………………

ii. Bainisha kifaa kimoja tu unachoweza kukitumia katika kujifunza kwa kucheza michezo sahili. ……………………………………………………

**MAJIBU YA KISWAHILI**

**Swali la 1**

i. Wazazi walisikia habari zake.

ii. Sisi tunasoma herufi mwambatano.

iii. Mtoto amekaa kwenye kochi.

iv. Wanafunzi wanaangalia runinga ukumbini.

v. Wote tunasoma kwa bidi.

**Swali la 2**

i. B
ii. C
iii. D
iv. B
v. D
vi. C
vii. B
viii. C
ix. A
x. D

**Swali la 3**

i. HADITHI
ii. HAPO
iii. ZAMANI
iv. PAMOJA
v. PAUKWA

**Swali la 4**

i. C
ii. D
iii. B
iv. E
v. A

**Swali la 5**

i. Mpitimbi
ii. Mboni, Baraka na Tumaini
iii. Mshangao (!)
iv. Maadui

## ENGLISH LANGUAGE ANSWERS

**Question 1**

i. That is a book.
ii. This is my bag.
iii. She is playing football.
iv. I am going home.
v. We are good pupils.

**Question 2**

i. C
ii. B
iii. C
iv. B
v. D
vi. B
vii. B
viii. C
ix. C
x. B

**Question 3**

i. D
ii. E
iii. A
iv. C
v. B

**Question 4**

i. Good
ii. Went
iii. Wrote

**Question 5**

i. Wakes up
ii. Brushes
iii. Goes
iv. Comes

**Question 6**

i. Twendepamoja primary school
ii. Five members
iii. Sikujua
iv. Agnes
v. Father

## HISTORIA YA TANZANIA NA MAAADILI

**Swali la 1**

i. C
ii. B
iii. C
iv. A
v. B
vi. A
vii. D
viii. C
ix. B

**Swali la 2**

i. B
ii. E

iii. D
iv. A
v. C

**Swali la 3**

i. Yanayositiri mwili
ii. Magofu
iii. Uzalendo
iv. Wajibu
v. Mwalimu mkuu msaidizi

**Swali la 4**

i. Watu watano (5)
ii. Watoto watatu (3)
iii. Dada
iv. Wazazi

**Swali la 5**

i. Shuleni
ii. Elimu
iii. Kusoma au kujifunza kwa bidi, kuwasikiliza na kuwaheshimu walimu, kutunza mali za shule,
iv. Ushirikiano wa kusoma kwa pamoja
v. Kujenga upendo, umoja na mshikamano

**Swali la 6**

i. Ukoo
ii. Asili moja
iii. Kutoa urithi na kupanga ndoa, kutoa mwelekeo wa maadili, kutoa ushauri, kushirikiana katika shughuli za kijamii
iv. Harusi, misiba
v. Kujua historia ya familia na kuepuka kuoana na mtu wa ukoo mmoja
vi. Mfumo wa ukoo wa baba

**JIOGRAFIA NA MAZINGIRA: SANAA NA MICHEZO**

**Swali la 1**

i. B
ii. B
iii. A
iv. B
v. A
vi. D

**Swali la 2**

i. Mawio na machweo ya jua
ii. Mashariki
iii. Kaskazini
iv. Magharibi

**Swali la 3**

i. Katografia
ii. Katografa
iii. Alama za ramani
iv. Google my maps, CAD, GIS

**Swali la 4**

i. Mitatu (3)
ii. Manne (4)
iii. Kaskazini
iv. Mbili (2)

**Swali la 5**

i. B
ii. D
iii. A
iv. C

**Swali la 6**

i. Kuangalia chini
ii. Noti
iii. Kuinua na kushusha mabega
iv. Koni
v. Toni

**Swali la 7**

i. Koni mzunguko
ii. Kuweka puto hewani

**Swali la 8**

i. Kukimbia na kijiko
ii. Kijiko kinaweza kushikwa mkononi, kijiko kinaweza kuwekwa mdomoni
iii. Msawazo na wepesi wa mwili

SAYANSI

**Swali la 1**

i. C
ii. D
iii. A
iv. C
v. D

**Swali la 2**

i. D
ii. A
iii. B
iv. E
v. C

**Swali la 3**

i. Protini

ii. Vitamini na madini
iii. Kabohaidreti au wanga
iv. Mafuta
v. Nyama na samaki
vi. Magimbi na viazi mbatata

**Swali la 4**

i. Hatari
ii. Mlango wa kutokea wa dharura
iii. Sumu au hatari
iv. Sakafu inateleza
v. Msongo mkubwa wa umeme
vi. Sehemu ya kuosha mikono

**Swali la 5**

i. Makundi matano
ii. Popo
iii. Kuzaa watoto
iv. Mapafu
v. Nyuzi za sentigredi 37

**Swali la 6**

i. Simu, kompyuta na kishikwambi
ii. Kujiamini na kujifunza kwa furaha au Kujifunza kwa kujitegemea na kwa kushirikiana

HISABATI

**Swali la 1**

i. Ishirini na nane elfu mia tatu na nne
ii. 8
iii. 7
iv. 400+0+50
v. 91
vi. XXII

**Swali la 2**

i. 939064
ii. 49580
iii. 1065
iv. 203856

**Swali la 3**

**i.** $^{5}/_{8}$
**ii.** $^{2}/_{5}$
**iii. 4**

**Swali la 4**

i. Gramu 6000
ii. Mililita 3000
iii. Mk 8
iv. Saa 2:300

**Swali la 5**

i. Pipi 32
ii. 5
iii. Miche 34

**Swali la 6**

i. Sm 28
ii. M 10
iii. Pentagoni
iv. Sm 48

LUSAELIMU.COM